*Mulika, Na. 43 (2), 351-370*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Urithi wa Vivuli: Kufichua Nyuzi za Baada ya Ukoloni katika Riwaya ya *Nguu za Jadi*

*Waithiru Kago Antony* [1]
Chuo Kikuu cha Laikipia

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.9

**Ikisiri**

Makala haya yanashughulikia urithi wa vivuli vya utawala wa kikoloni kwa kufichua nyuzi za baada ya ukoloni katika riwaya ya *Nguu za Jadi* iliyoandikwa na Clara Momanyi. Riwaya hii ilisomwa na mtafiti na baadaye masuala yaliyoonesha nyuzi za baada ya ukoloni yalidondolewa kwa kuzingatia lengo la makala haya. Lengo lenyewe lilikuwa kujadili jinsi ambavyo urithi wa vivuli huwekwa uchi kupitia nyuzi za baada ya ukoloni katika riwaya teule. Baadhi ya vivuli ni kama vile ukoloni mamboleo, ubaguzi, unyamazishaji, ufisadi, na uongozi mbaya. Kimsingi, makala haya yalichunguza namna madhara ya ukoloni yanavyoendelea kuathiri jamii baada ya kupata uhuru katika mfumo wa ukoloni mamboleo. Uchanganuzi wa makala haya uliongozwa na misingi ya Nadharia ya Baadaukoloni. Baadhi ya mihimili ya nadharia hii ni vita vya baada ya uhuru, ukoloni mamboleo, kuasi, na kutema. Uchanganuzi wa makala haya ulifanyika kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Njia kuu ya uchunguzi wa makala haya ilikuwa ya upekuzi-changanuzi wa yaliyomo. Ilibainika kuwa ubawa wa kibeberu ungali unayatawala mataifa ya ulimwengu wa tatu kupitia viongozi wa Afrika wanaotawaliwa na viongozi wa mataifa ya ulimwengu wa kwanza.

## 1.0 Utangulizi

Riwaya ya Kiswahili ina jukumu kubwa katika kuikosoa na kuirekebisha jamii (Jacob, 2020; Kar, 2024). Kupitia riwaya ya Kiswahili, waandishi huweza kuikosoa jamii kwa kuonesha uozo na uovu wake kama vile: ufisadi, uongozi mbaya, usaliti, ulevi, ulanguzi wa dawa za kulevya na anasa, ukosefu wa haki, kutokuwapo kwa usawa wa kijinsia pamoja na matatizo yahusuyo masuala ya mazingira (Helgesson, 2020; Guohuo, 2023). Kimsingi, fasihi hunuia kuchochea majadiliano na kusababisha watu kuchukua hatua za kujiendeleza wenyewe, mazingira yao, uchumi wao, uongozi na utawala wao pamoja na mifumo yao ya kijamii. Hivyo, fasihi ina wajibu wa kuikosoa na kuirekebisha jamii kwa kutoa mwelekeo kuhusu masuala muhimu ya jamii, na kusaidia kujenga uelewa na mabadiliko. Katika harakati za uelekezi na ukosoaji, fasihi huimarisha utambulisho wa jamii (Dewald, 2002; Bennett na Royle, 2024).

---

[1] **Baruapepe:** kagoantony3@gmail.com

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mwandishi Momanyi amesawiri vivuli[2] vya jadi vinavyofichua siri za utawala na uongozi wa mabeberu wa kisasa. Mtunzi amefanikiwa kusawiri vivuli hivi kupitia mila, mifumo ya uongozi mbaya pamoja na changamoto za kizazi kinachokumbwa na matatizo chungu nzima. Kupitia wahusika mbalimbali, mtunzi Momanyi amefanikiwa kumfafanulia msomaji kuhusu ulimwengu wa vikwazo na matumaini mapya katika ufichuzi wa nyuzi[3] za baada ya ukoloni kama vile mifumo mbalimbali inayounganisha jamii na urithi wa ukoloni. Mwandishi anadhihirisha njia mbadala za kuasi, kutema na kuvunja silisili zinazounganisha minyororo ya zamani na kuangaza njia mpya. Makala haya yamefafanua vivuli vya ukoloni kama vile: ukoloni mamboleo, ukabila na ubaguzi, unyamazishaji, uongozi mbaya, vita vya baada ya uhuru, ufisadi pamoja na athari za kumsahau mtoto wa kiume katika uongozi na maendeleo ya jamii.

## 2.0 Msingi wa Nadharia

Nadharia za uhakiki wa fasihi hugawika katika makundi matatu makuu; kundi la kwanza husisitizia ‘kinachosemwa’ (maudhui), la pili husisitizia kinavyosemwa (fani), na la mwisho husisitiza ‘ni nani anasema nini na kama nani’ (mtunzi na hadhira) (Waithiru, 2019). Nadharia ya Baadaukoloni hujikita kwenye kundi la kwanza.

Msingi wa Nadharia ya Baadaukoloni umo kwenye mawazo ya Waafrika ambao huishi kwenye mataifa yaliyowahi kudhulumiwa na mkoloni kutokana na uasi dhidi ya dhiki na matatizo chungu nzima ya miongo mingi iliyotangulia (Thiong’o, 1987; Blouin na Akrigg, 2024). Nadharia hii ilizuka katika mazingira ya ubaguzi, chuki na unyanyasaji wa mtawaliwa baada ya mkoloni kuondoka mamlakani. Nadharia hii imejizatiti kumrudishia mtawaliwa hadhi yake; hadhi iliyobomolewa na mkoloni. Kupitia mtazamo wa Kiafrika, nadharia imeonesha kwamba falsafa zilizokuwa zikitumiwa na wakoloni kuwatawala Waafrika zilikuwa za uheke. Hii ni nadharia inayouauni ulimwengu wote kupalilia mazoea na mielekeo ya kidemokrasia (Mwirabua, 2014). Loomba (2015) anapambanua kuwa katika dhana ya baadaukoloni, msomi anaruhusiwa kuzungumza kuhusu tofauti za kimila, kiitikadi na kidesturi lakini si kuhusu dhuluma za kiuchumi. Mihimili mitatu iliongoza uhakiki wa makala haya. Mihimili hiyo ni ukoloni mamboleo, vita vya baada ya uhuru na uhuluti. Singh (2021), Blouinn na Akrigg (2024) pamoja na Nanda (2025) wanafafanua kuwa ukoloni mamboleo ni dhana inayotumiwa na

[2] Vivuli ni dhana inayorejelea vipengele vinavyoendelea kuwapo katika nyanja za kijamii, kisiasa, kitamaduni na kisaikolojia katika jamii zilizowahi kutawaliwa na mkoloni katika kipindi cha ukoloni mkongwe. Vivuli hivi huwakilisha mvutano ambao ungali tata, kuvurugika kwa tamaduni au hata majeraha na makovu ya kihistoria. Huu ndio ujadi unaojadiliwa katika makala haya.

[3] Nyuzi ni istilahi inayoashiria masuala mbalimbali ya baada ya ukoloni yanayoshikamana na kujenga hadithi, maana na hulka za wahusika pamoja na jamii kwa ujumla kwenye riwaya iliyochambuliwa katika makala haya.

wakosoaji wa baada ya enzi ya ukoloni dhidi ya mataifa yaliyostawi kuingilia masuala ya mataifa yanayoendelea. Aidha, wanaongeza kuwa ni wakati ambapo Mzungu aliondoka na Waafrika walioshika hatamu wakaanza kuendeleza nyenzo zilezile za Mzungu za utawala. Gandhi (2020), Yamamura na Yu-Chieh (2023), Cardina (2024) pamoja na Sioh (2024) wanajadili kuwa vita vya baada ya uhuru hutumiwa kuelezea changamoto, migogoro na mizozo ambayo jamii nyingi za maeneo yaliyopata uhuru zilipitia baada ya kuondoa utawala wa kikoloni. Licha ya mapambano ya kijeshi, vita hivi huhusisha mizozo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni ambayo huibuka katika mchakato wa mataifa hayo wa kujijenga kiuchumi.

Katika makala haya, migogoro michache mikuu imejadiliwa mintarafu ya lengo la makala. Mathalani, kutoelewana kuhusu mifumo ya utawala katika vita vya kisiasa, kuna mgawanyiko wa kikabila unaosababishwa na jadi za kikoloni, suitafahamu kati ya tamaduni za jadi na za kisasa pamoja na ukosefu wa mshikamano wa kitaifa kutokana na ukosefu wa utambulisho katika vita vya kijamii. Aidha, kuna ukosefu wa usawa wa kiuchumi ambapo tabaka fulani linaendelea kutajirika huku tabaka lingine likiendelea kudidimia kwenye ufukara pamoja na unyonyaji wa rasilimali za kitaifa katika vita vya kiuchumi. Isitoshe, kuna mvutano kati ya maadili ya jadi na ushawishi wa Magharibi; migogoro ya lugha pamoja na kupotea kwa utambulisho wa kitamaduni kutokana na athari za ukoloni katika vita vya kitamaduni. Kwa mujibu wa Waithiru (2022), uhuluti ni hali ambapo masuala ya mkoloni na yale ya mtawaliwa, mathalani, tamaduni zao, zinashikamana na kuzalisha utamaduni mpya. Nadharia hii inadhihirisha juhudi za 'ulimwengushaji' wa usomi wa kimagharibi. Uhuluti unaonesha namna udhibiti wa utamaduni wa nchi za Kimagharibi unavyovunja tamaduni za Kiafrika kwa mfano, kutokana na miigo na takriri za nchi tawaliwa. Maingiliano haya yamesababisha kuwapo kwa 'utamaduni mseto' (Wamitila, 2002, 2003; Waithiru, 2024). Kutokana na chimbuko la Nadharia ya Baadauukoloni, kuna haja ya kuangaza uozo wa uongozi, utawala na maadili ya jamii kupitia uhakiki wa kazi za fasihi kwa kuongozwa na mihimili yake inayoendelea kukua na kuwanda kiuamilifu (Koobak na wenzake, 2022).

## 3.0 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti wa Makala

Kipengele hiki kinawasilisha mjadala wa matokeo ya utafiti wa makala haya. Mjadala huu uliongozwa na mihimili mitatu ya Nadharia ya Baadaukoloni, mintarafu ya lengo kuu la makala. Maeneo saba yamefanikiwa kubainisha na kujadili namna ambavyo urithi wa vivuli huwekwa paruwanja kupitia nyuzi za baada ya ukoloni katika riwaya ya *Nguu za Jadi*. Maeneo haya ni pamoja na ukoloni mamboleo, ukabila na ubaguzi, unyamazishaji, uongozi mbaya, vita vya baada ya uhuru, ufisadi, na athari za kumsahau mtoto wa kiume katika uongozi na maendeleo ya jamii.

**3.1 Ukoloni Mamboleo**

Mjadala kuhusu ukoloni mamboleo umejikita katika mhimili wa ukoloni mamboleo wa Nadharia ya Baadaukoloni. Mtemi Lesulia anawakilisha viongozi wengi barani Afrika ambao hutawala kupitia mfumo wa ukoloni mamboleo. Katika mataifa mengi fukara ulimwenguni, vigogo kama vile marais huchukua sheria mikononi mwao kwa kupuuza katiba husika. Hali hii inawiana moja kwa moja na utawala uliowahi kuenedelezwa na mkoloni katika mataifa yaliyowahi kumilikiwa naye ulimwenguni. Mathalani, kauli za Mtemi Lesulia zinachukuliwa kama sheria za taifa. Badala ya viongozi barani Afrika kuimarisha amani, udugu na umoja wao; hupalilia woga baina ya wananchi kwa kuwadhulumu. Hakika, huu ni utawala unaodhibitiwa na kanuni za ukoloni mamboleo. Aidha, viongozi hupalilia uhasama baina ya jamii tofauti ili kuwapa nafasi mwafaka ya kuwatawala kwa hila chini ya mfumo wa tenga-tawala. Hali hii inafungamana na mhimili wa ukoloni mamboleo wa Nadharia ya Baadaukoloni. Mfumo huu wa ukoloni mamboleo huwapa nafasi vikaragosi hawa kuwapunja wananchi na kufuja mali ya umma (Loh na Sen, 2018).

Ukoloni mamboleo huimarisha uhasama baina ya wananchi kupitia chuki, ukabila, na elimu isiyoimarisha suluhu ila kuanika na kupapasa changamoto tu. Hili linawiana na kauli ya Oliver (2016) kuwa lengo kuu la ukoloni mamboleo ni kuimarisha utawala wa Mzungu katika kipindi cha baada ya usasa ulimwenguni. Kusudi la kuwagawa watawaliwa katika makundi ya kikabila ni kuimarisha utawala wa hila pamoja na kudumisha umaskini. Siasa za umaskini na majina ni silaha madhubuti ambayo hutumiwa na viongozi wengi barani Afrika. Vitengo vya usalama hujumuisha watu wa kabila moja kwa kiwango kikubwa zaidi (Omolo, 2002), kusudi likiwa viongozi waweze kudhibiti na kuvitumia vitengo vya usalama kuwatisha na kuwadhulumu watawaliwa kama alivyokuwa akifanya mkoloni ili kuwadhibiti watawaliwa. Mathalani, mwandishi Momanyi anaeleza: “Jeshi la nchi lilisheheni vijana kutoka katika jamii ya Wakule” (uk. 44). Tatizo kuu la uongozi huu wa mabeberu wa kisasa katika mfumo wa ukoloni mamboleo ni kuwa, wengi wanaoajiriwa katika idara na sekta mbalimbali za serikali hudorora kistadi. Kutokana na hili, ajali huwa jambo la kawaida, maafa huwa tukio la kila siku na elimu hudhoofika katika msingi wa bora elimu wala si elimu bora kama ilivyorithiwa kutoka kwa mkoloni. Mathalani, katika nchi ya Matuo, taifa lilididimia kiuchumi kwa sababu miradi ya kuwawezesha wananchi kujiinua kiuchumi ilifurika ufisadi, ukabila na ubaguzi. Nafasi chache za ajira zilizopatikana walipewa jamaa na marafiki wa viongozi wasio na ujuzi wala maarifa. Hili linawiana na mhimili wa ukoloni mamboleo.

Vikaragosi wa mataifa yaliyowahi kuyatawala maeneo tofautitofauti kama makaoloni yao, wanaendeleza ukoloni mamboleo kwa kutumia woga kama silaha ya kuwanyamazisha raia. Mhusika Mrima anadhihirisha hili anapomuasi mke wake – Mangwasha – kuwa, asicheze na wazo la kukutana na Mtemi Lesulia.

Woga wa Mrima unatokana na dhuluma za Mtemi Lesulia kwa Waketwa. Hili linawiana na kauli ya Thiong'o (2009) kuwa viongozi waliochukua hatamu za uongozi baada ya mkoloni kubanduliwa mamlakani hutumia nyenzo zilezile za unyama, ubaguzi na utabaka. Huu ni msingi wa mhimili wa ukoloni mamboleo.

Kando na kuwaogopesha wananchi, vikaragosi hawa huwa wanateka nyara wapinzani wao wa kisiasa ili waendelee kutawala kwa hila huku wakiwatenganisha na kuwagawa raia. Kabla ya uchaguzi wa kitaifa nchini Matuo, Lonare alikuwa na ruwaza safi ya kuwaauni wananchi wote wa taifa la Matuo bila ubaguzi wala unafiki. Hekima ya Lonare iliwatia Wakule hofu na hili lilimfanya Mtemi Lesulia kuwatuma majambazi wakamwangamize. Mara kadhaa Lonare alinusurika kifo kutokana na mashambulizi ya majambazi hao. Waliposhindwa kumwangamiza, Mtemi Lesulia alihakikisha kuwa Lonare pamoja na vinara wakuu wa chama chake cha kisiasa walitekwa nyara. Hili lilimhakikishia Mtemi Lesulia kuchaguliwa bila kupingwa. Haya yote hufanikishwa siyo tu na hila za viongozi bali pia raia ambao huendelea kufaidi mali ya umma kwa kuficha uozo na uovu wa viongozi dhalimu chini ya mfumo wa ukoloni mamboleo. Mtunzi Momanyi anapendekeza kuwa suluhu ipo katika kuuaunika ukatili wa vikaragosi hawa mchana peupe ila si kuuficha ndani ya ukoloni mamboleo. Mfumo huu wa udhibiti wa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni unaotekelezwa na mataifa yenye uwezo dhidi ya yale yaliyo huru, huendeleza athari za ukoloni kwa njia zisizo wazi kama zile za ukoloni mkongwe. Hata hivyo, kuna haja ya kuubomoa mfumo huu, hususani katika mataifa ya Afrika kama anavyofafanua Waithiru (2024: 167) kuwa:

> … hatuhitaji mawazo ya kigeni wala utamaduni wa Mzungu kujikomboa kimawazo, kiuchumi, kijamii wala kisiasa ila tunahitaji mawazo yetu; lugha yetu; utamaduni wetu; na mazingira yetu ya AFRIKA!

### 3.2 Ukabila na Ubaguzi

Vikaragosi wa mataifa kwasi au wa ulimwengu wa kwanza huwaletea wananchi madhara mengi. Baadhi ya dhiki wanazopitia raia ni pamoja na ukosefu wa ajira hasa kwa vijana waliohitimu katika taaluma mbalimbali, ubaguzi, ukabila, na zingine nyingi. Hali hii inafungamana na mhimili wa vita vya baada ya uhuru wa Nadharia ya Baadaukoloni. Ubaguzi hurudisha maendeleo nyuma na hulididimiza taifa kwenye giza la kutojifahamu wala kujiweza kiuchumi, kisiasa na kijamii (Malcolm, 2024). Uchumi katika mataifa mengi ya ulimwengu wa tatu huendelea kuzorota chini ya utawala wa vikaragosi hao. Miradi ambayo huanzishwa hunuia kuwanufaisha vikaragosi hao na wafuasi kutoka kabila lao ila si wananchi kwa jumla. Hali hii husababisha maafa kwa kuwa nafasi chache zinazopatikana za ajira hupewa watu wasiokuwa na ujuzi wala maarifa. Hali hii ni sawa na jinsi mkoloni alivyokuwa akiteua viongozi wa vijiji nyakati za ukoloni mkongwe kwa upendeleo (Coghe, 2017).

Hivyo, nyayo zilezile zilizofuatwa na mkoloni ndizo zilizofuatwa unyounyo na vikaragosi hawa. Kwa mfano, mtunzi Momanyi anaeleza, "Halikuwa jambo la kushangaza kumwona karani akiajiriwa kuwa daktari wa meno na muuguzi akifanya upasuaji hospitalini. Wagonjwa hospitalini wakawa wanafariki kiholela" (uk. 44). Kutokana na ukabila, ubaguzi na upendeleo, vikaragosi hawa husababisha hasara kubwa kwa taifa. Ikizingatiwa kwamba wao wenyewe huwa hawajiamini uongozini, huwaajiri watu wasio na fununu kuhusu taaluma zao. Hii ndio sababu Mtemi Lesulia aliwateua wanajeshi wenye mafunzo duni na manahodha waliopungukiwa kitaaluma. Matokeo yake ni kuwa marubani wengi wa kijeshi waliangusha ndege ovyo ilhali manahodha walipasua vyombo kwenye miamba kama ibada. Aidha, ajira kwa walimu wasiohitimu katika masomo ni jambo la kusherehekewa katika mataifa duni. Kwa kawaida, serikali kwa ujumla hupigia upatu mtindo wa bora elimu ila siyo elimu bora. Hili linawiana na nguzo ya ukoloni mamboleo.

Tatizo la ukabila hudidimiza maendeleo endelevu katika mataifa mengi duni hasa barani Afrika. Vijana wengi barani Afrika hukumbwa na ukosefu wa ajira. Mwandishi Momanyi anasawiri hali hii anaposema, "Hivyo, majopo hayo ambayo yaliongozwa na Wakule, yalitazama majina. Aliyekuwa na jina la Kiketwa aliondolewa katika orodha ya watakaohojiwa katika kazi za ngazi za juu. …Siasa za majina zikashamiri katika utawala wa Mtemi Lesulia" (uk. 44 – 45). Sera dhoofu za uongozi na utawala huchangia uchafuzi na uharibifu wa mazingira wenye mabadiliko yenye madhara ya kudumu katika mataifa yanayoongozwa na vikaragosi. Katika mataifa mengi duni ulimwenguni, hususani yaliyowahi kutawaliwa na mkoloni, sera za ubaguzi husababisha ufisadi wa kimazingira ambapo misitu hufyekwa bila kujali. Ufyekaji huu ovyo wa miti husababisha mabadiliko ya misimu ambapo mvua hupungua na chemchemi za maji hukauka. Uhalisi huu husababisha wakulima kuchanganyikiwa kwa kutojua msimu upi ni mwafaka wa upanzi; hivyo, mavuno hupungua na njaa hushamiri. Punde tu njaa ibishapo hodi, mabepari ambao huwaabudu vikaragosi huhodhi vyakula muhimu na kuviuza kwa bei ya juu zaidi.

Kwa misingi hiihii, mabepari hawa baada ya kukata mti wa mwisho huchimba mchanga kwa mafungu na kuuza pia kwa bei ya juu sana. Mashimo makubwa yanayozalishwa na shughuli hii huwa chanzo cha maafa kwa watoto wengi wa wananchi duni. Hii ni kwa sababu, mvua zisizoaminika zinyeshapo hufurisha mashimo hayo na maji ambayo huwazamisha watoto wanapojaribu kujiburudisha kwa kuogelea mle. Mwandishi anadhihirisha hili anapofafanua kuwa:

> Matajiri wakaajiri vibarua wa kuchimba na kukusanya mchanga kwa mafungu ili wauze. Mashimo makubwa yakasalia kuwa wazi baada ya mchanga kuvunwa. Mvua ziliponyesha, yakajaa maji. Maji hayo yakakamia kuzamisha watoto wa maskini walioogelea mahali hapo na

> makabwela walevi waliosepetukia mashimoni. Mashimo hayo basi yakawa hatari kwa usalama wa wananchi (uk. 46).

Hakika, matajiri katika mataifa fukara duniani huwaajiri watoto na vijana wa maskini katika vibarua vya kijungujiko huku wakivuna mapato tele zaidi ya asilimia elfu moja ya faida. Hali hii inasawiriwa na mwandishi Momanyi anayeonesha namna matajiri wanavyowaajiri vijana na watoto wa maskini waliokosa fursa ya kuendelea na masomo kutokana na ukosefu wa karo. Umaskini unawafanya watoto na vijana hawa kukaa juani wakipasua mawe na kutengeneza kokoto. Kutokana na hili, mazingira yanaharibiwa zaidi. Ulafi wa matajiri unasababisha kubomolewa kwa vilima. Baruti zinawaziba masikio wenyeji wanaoishi karibu na machimbo ya mawe huku wengine wakipatwa na maradhi ya kupumua. Baadhi ya wananchi wanahamishwa.

Ubinafsi na uchoyo wa matajiri unafanya shughuli zinazosababisha mabadiliko ya kudumu katika mazingira. Kwa mfano, nchi ya Matuo inapata mazingira mapya yaliyonajisiwa baada ya baadhi ya matajiri kuingilia mito na vijito huku wakidhibiti mikondo ya mito ili kuyatumia maji yale kuyanyunyizia mashamba yao makubwa. Hali hii inasababisha ukame kwa wananchi baada ya mito iliyosalia kumilikiwa na matajiri wachache. Maradhi, njaa na maafa yanashamiri miongoni mwa wananchi wa Matuo. Hakika, changamoto hizi hushuhudiwa kila uchao na wananchi katika mataifa mengi barani Afrika. Hali hii inafungamana na mhimili wa vita vya baada ya uhuru ambapo wananchi hukumbana na matatizo tele katika vita vya kiuchumi na kijamii. Hili linasababisha wananchi wakiongozwa na vijana kuandamana mara kwa mara kutokana na utamaushi unaozalishwa na vikaragosi wao (Falola, 2024a, 2024b).

Hili linawiana na kauli ya akina Engbersen (2020), Knight (2020) na Muhammad na wenzake (2023) kuwa, ukosefu wa ajira, mabadiliko ya tabianchi, ukosefu wa matumaini baina ya wananchi, ufisadi, uongozi mbaya na ulofa ni propela inayoisukuma na kuichochea hasira na dhiki zinazowakumba Waafrika na wanyonge kwa ujumla. Ukosefu wa ajira huwasababishia wananchi hasa vijana kukata tamaa na kutafuta njia za kujikimu ambazo mara nyingi huwa hasi. Mathalani, ukosefu wa ajira huwatumbukiza vijana kwenye matumizi ya dawa za kulevya, pombe haramu na wizi wa kimabavu huku wengine wakibuni njia za kuwalaghai watu kupitia mitandao ghushi (Harris, 2024). Aidha, ni dhahiri kuwa kuna haja ya kuchukua hatua madhubuti zenye nia njema za kulinda mazingira na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Njaa, maradhi na dhiki zinazotokana na mabadiliko haya huwanyima vijana matumaini ya maisha bora madhali hukumbwa na hali ngumu ya kiuchumi na kijamii. Ufisadi na umaskini ambao huzalishwa na ukabila na ubaguzi ulimwenguni, huchangia uadimikaji wa sera madhubuti za maendeleo endelevu. Mwandishi Momanyi anaonesha hali hii anapofafanua:

> Ukosefu wa matumaini ya kuishi ulianza kuhasiri mifumo ya kijamii. Asasi ya familia ikaathirika sana pale mizozano ya kifamilia ilipokithiri. Waume kwa wake wakawa makatili kiasi cha kuangamiza makinda yao. Mume akamgeukia mke na kumchinja naye mke akafanya vivyo hivyo. … upendo ukatoroka kupitia dirishani, uhitaji ulipobisha mlangoni. Taasisi na mashirika ya serikali yakamilikiwa na mitandao ya wezi. Wakaiba, wakanyonga na kupokonya (uk. 47).

Ukabila, ubaguzi, umaskini na ufisadi ndiyo masuala yanayoimarisha ukoloni mamboleo ambao ndio ujadi wa sasa unaokemewa na mwandishi wa *Nguu za Jadi*. Ukoloni mamboleo hupigwa vita na wananchi katika mataifa duni. Hii ni kwa sababu husambaratisha nchi na kuwagawa wananchi katika makundi ya walio navyo na wasio navyo, yaani walalaheri na walalahoi. Hili linalandana na mihimili ya vita vya baada ya uhuru pamoja na ule wa ukoloni mamboleo. Ujadi wa kisasa unazalisha madhara kama vile wasichana wachanga kuzurura kwenye barabara za miji huku wakivibeba vitoto vyao migongoni wakiomba chakula. Ujadi huu unazalisha vigoli wasioweza kuwa wanawake wa kutunza familia zao; unazalisha kizazi kilichopotea kabla hata ya kuzaliwa. Ubaguzi huu hudhihirika katika vijiji, mitaa na miji mbalimbali ulimwenguni. Ukabila hukita mizizi kama zao la ukoloni mamboleo katika mataifa mengi fukara ulimwenguni, hususani ya ulimwengu wa tatu. Hali hii inafungamana na nguzo ya ukoloni mamboleo. Katika *Nguu za Jadi* mwandishi Momanyi kupitia wahusika Mtemi Lesulia na Sagilu, anadhihirisha ukabila na ubaguzi. Katika viwanda vilivyomilikiwa na hawa wawili, waajiriwa wote walikuwa Wakule pekee.

### 3.3 Unyamazishaji

Ni hali ambapo mtawaliwa ananyimwa haki zake za msingi kama vile ya kuishi, kuzungumza na kutoa maoni huru, kutembea, kuabudu, kula, kuelimika, kufahamu kujihusu na kuhusu uongozi na utawala pamoja na haki ya kutumia lugha mja apendayo kwa kuendeleza utamaduni wake. Mjadala katika sehemu hii uliongozwa na mihimili ya ukoloni mamboleo, vita vya baada ya uhuru pamoja na uhuluti ya Nadharia ya Baadaukoloni. Unyamazishaji ndio uti wa mgongo wa mhimili wa ukoloni mamboleo na kigezo kikuu katika mhimili wa vita vya baada ya uhuru. Aidha, ili mhimili wa uhuluti ufanikiwe katika kuimarisha utamaduni mgeni katika jamii zenye utamaduni wake, unyamazishaji huchangia kwa kiasi kikubwa katika kulazimisha ukubalifu wa utamaduni mgeni (Rubin, 1988; Kamrava, 1999; Gibson, 2006; Brear, 2020). Mhusika Lonare katika *Nguu za Jadi* anadhihirisha namna viongozi dhalimu kama Mtemi Lesulia wanavyowanyamazisha wapinzani wao. Lonare anasifika katika biashara ya usafiri na serikali ya Mtemi Lesulia inamnyanyasa na kumnyamazisha kupitia biashara hii ingawa bila mafanikio ya kudumu. Mwandishi Momanyi anafafanua kuwa Lonare alihangaishwa na kunyimwa utulivu na askari kwa tuhuma za visingizio. Magari yake ya usafiri yalizuiliwa katika vituo tofautitofauti vya polisi nchini Matuo bila kosa lolote. Madereva wa Lonare nao walishikwa na kushtakiwa makosa

yasiyokuwapo na kutozwa faini za kudhalilisha. Baadhi yao walinyang'anywa leseni za kuendesha magari bure. Hata hivyo, Lonare alivumilia na kuwa na imani kuwa dhuluma hizo zingefika ukingoni siku moja.

Wahusika Mtemi Lesulia na Sagilu wanajaribu mbinu aina aina za ukatili kumnyamazisha Lonare. Walihusudu umaarufu wake na biashara zake. Walimpangia njama za kumwangamiza si haba. Wakati mmoja, waliwatuma magaidi kumuua Lonare lakini badala yake, watu wale wakamwendea Lonare na kumwonyesha malaki ya hela walizokirimiwa ili wamuue. Lililowatia kiwewe Mtemi Lesulia na Sagilu ni kuwa, Lonare alikuwa na ari, bidii na nidhamu ya kuwania kiti cha Mtemi nchini Matuo. Lonare alipata msukumo huu kutokana na dhuluma, ubaguzi na manyanyaso yaliyokuwa yakiwakumba wananchi wa Matuo kila uchao. Kutokana na uongozi dhoofu, uchumi ulikuwa ukisambaratika kwa kasi, rasilimali ya taifa ilikuwa ikinajisiwa na matajiri na viongozi wezi. Utandu wa mahasidi hao ulizidi kupanuka kila siku. Azma ya Lonare ya kuwania kiti cha Mtemi ilitokana na mapenzi yake kwa watu wa nchi ya Matuo ila si tamaa ya pesa na cheo.

Wafuasi wa Lonare wanatishwa kwa kutakiwa kuhama kutoka makazi yao. Lengo kuu likiwa kumpunguzia Lonare kura wakati wa uteuzi na uchaguzi ufikapo ilimradi Mtemi Lesulia asalie uongozini na kuendelea kuwadhulumu na kuwanyima wananchi haki zao. Viongozi dhalimu na vikaragosi wa mataifa tajiri yaliyowahi kuyatawala mataifa duni hutumia unyamazishaji kama ala ya kuwaondoa wapinzani wao wazalendo kwa taifa lao. Mtunzi Momanyi anadhihirisha hili kupitia mhusika Lonare anayeeleza: "Hii ndiyo maana amefanya maisha yangu kuwa magumu kabisa. Ananichunga kama kuku mgeni. Ameniundia vigwena, kila nipitapo wananiandama" (uk. 54). Hali hii inafungamana na mhimili wa ukoloni mamboleo.

Ndoto ya kutisha anayoota Mangwasha inaashiria wazi namna ambavyo vikaragosi hutumia vitisho kuwanyamazisha wafuasi na wananchi wao kwa ujumla, kufuata na kuzingatia maagizo yao. Ukubwa wa jinyama lile unaashiria uwezo wa vikaragosi wa kutumia mamlaka watakavyo bila kuzingatia sheria. Uwezo huu unatokana na mikopo ya kiutumwa wanayolazimishwa kuchukua na mataifa kwasi ya Ulaya, Marekani, Uchina na Urusi. Weusi wa jinyama lile unadhihirisha kuwa linatawala bara la Afrika. Vilevile, inadhihirika kuwa Waafrika wana uwezo wa kuyaongoza na kuyalinda mataifa yao lakini ufisadi, tamaa na ubinafsi wa kujitajirisha huwapumbaza. Udhaifu huu hutumiwa na viongozi wa mataifa ya ulimwengu wa kwanza kuwathibiti vikaragosi hawa wapendavyo. Vikaragosi hawa badala ya kutumia uwezo wao kuyasaidia mataifa yao huutumia kujiendeleza wenyewe kiuchumi kwa kuyatumia mali ya umma na asasi za serikali kwa manufaa yao wenyewe.

Hakika hili linafungamana na kauli ya akina Johnston na wenzake (2019) na Jones (2022) kuwa, bara la Afrika lina uwezo wa kujiendeleza zaidi ya upeo wa mataifa ya ulimwengu wa kwanza lakini changamoto kama vile ufisadi, tamaa, ubinafsi na siasa za ukabila na umaskini huligubika gubigubi kiwango kwamba linashindwa kupumua kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wananchi kama Mangwasha ambao huweza kuvunja minyororo ya tamaa, ubinafsi na unyamazishaji huwa adimu barani Afrika. Mangwasha baada ya Sagilu kujaribu kumnyamazisha kimapenzi kwa kutumia noti mpya za shilingi elfu anazirusha nje zinapeperushwa na upepo. Kando na vitisho vya kuogopesha vikaragosi katika mataifa duni hutumia hela za miradi na zinazokopwa kuwahonga wapinzani kwa lengo la kuwanyamazisha. Mangwasha anapojaribu kujitetea mbele ya lile jinyama lenye machonge makubwa ya meno na ulimi mrefu mwekundu linatoa noti mpya za shilingi elfu kutoka jinywani lake. Lengo kuu likiwa kumnyamazisha Mangwasha. Hata hivyo, badala ya Mangwasha kuchukua zile hela analirushia jinga la moto kwa nguvu zake zote linalopasukia usoni mwa jinyama lile na linaangamia.

Isitoshe, vikaragosi hawa wanatumia vijana wa maskini kuwachomea baadhi ya wananchi makazi yao kama njia ya kuwanyamazisha kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mathalani, mtaa mzima wa Matango unateketea usiku mmoja. Kwa mujibu wa baadhi ya wenyeji, moto ule unasababishwa na vijana waliotumia mafuta ya petroli. Sihaba kwa kutumia gari jekundu anatumwa na akina Sagilu na Mtemi Lesulia kuwafikisha vijana wale mle mtaani Matango kuzichoma nyumba za Waketwa kwa kutumia mafuta ya petroli yaliyokuwa kwenye mitungi na vibuyu. Unyamazishaji huu unapalilia umaskini, chuki na maangamizi kwa ujumla. Unafanikishwa na uratibu kabambe wa vikaragosi. Mhusika Mbungulu anadhihirisha hili anaposema: “Bila shaka ni wao ambao walizima umeme ili watekeleze udhalimu ule. Hii ni haramu mutlaki” (uk. 67).

### 3.4 Uongozi Mbaya

Sehemu hii imejadiliwa kwa kuongozwa na mhimili wa ukoloni mamboleo wa Nadharia ya Baadaukoloni. Uongozi mbaya huzalisha matajiri wachache na wanyonge chungu nzima ulimwenguni. Mwandishi Momanyi anasawiri uhalisi huu kupitia mhusika Mbwashu ambaye ni kikaragosi cha Mtemi Lesulia. Mbwashu alikuwa mfanyabiashara maarufu mjini Taria aliyemiliki msururu wa maduka na majumba ya ghorofa aliyowapangisha wakwasi wa Matuo. Pia, alimiliki majumba ya kifahari katika mtaa wa Majuu aliyowapangisha wakuu wa serikali, mabalozi kutoka nchi za nje na wafanyabiashara wa kimataifa. Mbwashu alikuwa tajiri aliyetajirishwa na jasho la wananchi wa taifa la Matuo. Hakujali mustakabali wa taifa lao kamwe. Ubinafsi na tamaa zilimfanya kuwa kikaragosi asiyejali maisha ya wanyonge wa Matuo. Aidha, yeye pamoja na vikaragosi wengine walifisidi taifa bila kusaza hata thumni. Mwandishi Momanyi anadhihirisha hili anapoeleza:

> Mama huyu akishirikiana na vigogo wengine matajiri walifisidi mapato ya nchi. Ndio waliosababisha mfumko wa bei kila wakati. Hawa ndio waliokuwa wakididimiza uchumi wa nchi. Waliagiza bidhaa kutoka nje ya nchi na kukataa kulipa ushuru. Ndio waliotumia maafisa wa ngazi za juu serikalini kuagiza bidhaa ghushi ambazo hawakulipia ushuru (uk. 68).

Uongozi mbaya huimarisha taasisi zisizowajibikibia majukumu na uamilifu wao. Hali hii inawiana na mhimili wa ukoloni mamboleo. Mathalani, ofisi za upelelezi nchini Matango zimesaki wafanyakazi wazembe ambao kazi yao ni kufurisha matumbo yao binafsi. Vikaragosi huwaona wananchi kama panya ila sio kama wanadamu. Waketwa wanaporejea makwao na kukita mahema, uongozi unasambaza vijikaratasi vyenye maandishi ya kuwataka wahame. Mtemi Lesulia anamwambia Sagilu kuwa: "Wale panya wamesharudi katika makao yao tena" (uk. 78).

Viongozi dhalimu huendeleza mbinu na mikakati dhaifu ya uongozi hasa katika mataifa fukara ulimwenguni. Mtemi Lesulia anatumia njama za hila kuufifisha umaarufu wa mpinzani wake – Lonare. Anawahonga vijana wachache kwa lengo la kuwapa jukumu la kuharibu zoezi la upigaji kura. Aliwaelekeza kuwa wavuruge shughuli ya upigaji kura siku ya uchaguzi katika vituo vyote vilivyokuwa na idadi kubwa ya wafuasi wa Lonare. Walitakiwa wazue rabsha kali zaidi katika vituo vya Majengo na Matango. Mbinu hii hutumiwa na viongozi wengi waovu ambao hutumia ufisadi, ubaguzi na dhuluma mbalimbali katika uongozi na utawala wao wa kidikteta. Bara la Afrika huongoza katika utekelezi wa unyama wa aina hii na vikaragosi wanaoongoza mataifa mengi (Amis, 2020; Galperin na Scheepers, 2025). Badala ya kutumia uwezo na mamlaka yao kuhakikishia wananchi usalama wao na wa taifa kwa ujumla, hutumia vyombo vya usalama kujinufaisha wao wenyewe. Mathalani, Mtemi Lesulia anaeleza kuwa:

> Lazima Sagilu achukue kiti cha Matango. Hapo mjaribu sana kuwa na vurugu na kuharibu kura za mpinzani wake. Ulinzi mkali wa serikali utakuwepo. Tayari nimeshatoa maagizo kwa vikosi vyangu (uk. 128).

Kutokana na udhalimu wa Mtemi Lesulia, anamteua rafiki yake mkubwa wa karibu – Sagilu – kuwa mwenyekiti wa Halmashauri ya Mapato katika nchi ya Matuo. Hali hii inafungamana na mhimili wa ukoloni mamboleo. Sagilu anafuata nyayo za rafiki yake za ubinafsi, ukatili na ubadhilifu. Hakuaminika kutokana na kubadilika kwake kila mara mithili ya lumbwi. Viongozi wengi barani Afrika huwadharau maskini, huabudu utajiri wao na huyanajisi mataifa yao kiuchumi. Mathalani, Sagilu anawadharau maskini, amejaa kiburi na majitapo na ana ukatili usiomithilika. Wananchi wanaompiku kimawazo anawafanyia hila na kuwadhalilisha kibiashara.

Kutokana na uongozi dhalimu, uchumi wa nchi ya Matuo unadhoofika kabisa. Tunaelezwa: "Waliendeleza ubeberu wa kiuchumi nchini huku nakisi ya bajeti ikipanda kila mwaka. Kupanda kwa bei za bidhaa nchini Matuo kukawa ni jambo la kawaida." (uk. 17). Suala la kutowesha au kuficha bidhaa kisha kuziuza kwa faida maradufu hatimaye ni la kawaida katika mataifa mengi fukara duniani. Viongozi huyapuuza masilahi ya wananchi na taifa kwa ujumla. Hili huchangiwa kwa kiasi kikubwa na ufisadi na kutowajibika kwa viongozi. Mathalani, Sagilu anauza ngano kwa bei ya juu baada ya kuificha bandarini miezi kadhaa. Ngano yenyewe ilikuwa imeagizwa kimagendo bila kuilipia ushuru. Isitoshe, anaagiza mali ya thamani kubwa bila kulipia ushuru kisha kuzisambaza bidhaa zile ghushi nchini Matuo bila kujali siha ya umma.

Uongozi mbaya huchangia uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Mazingira ya mataifa mengi duni ulimwenguni yamesheheni uchafu chungu nzima. Maradhi ya mapafu, pumu, kuendesha, kikohozi, upele na hata saratani hushamiri na matokeo yake huwa vifo vinavyoweza kuepukika vya watu, wanyama na mimea. Katika mtaa wa Majaani, uchafu umesaki pomoni. Mtunzi Momanyi anasisitiza kuwa Majaani si eneo la kuishi kwa kuwa limesheheni wahuni na wachopozi. Limezagaa wazururaji na wauaji wanaotoa roho za watu ovyo na ndipo takataka zote za mji zinapomwagwa. La kutamausha katika mataifa duni ni kuwa, ukosefu wa ajira huwafanya wananchi wengi kuwa maskini hohehahe. Ufukara huu huwafanya wenyeji kujituma kwenye vilima vya marundo ya taka ya maji huku wakisaka tonge kwa kuokota chupa za plastiki na kuchakura taka ili wazichuuze mjini baadaye. Eneo lile la Majaani lilikuwa karimu kwa kuwakaribisha watu kutoka mbali kwa harufu kali ya uvundo wa uozo wa aina aina ya taka. Kutokana na uhitaji, binadamu walioishi pale Majaani walimenyana na kuvutania makombo ya vyakula kutoka kwenye jaa hilo kuu na kunguru, majibwa na yenyewe kwa yenyewe. Uongozi mbaya unawabadilisha raia wa nchi kuwa watumwa na wakimbizi nchini mwao.

### 3.5 Vita vya Baada ya Uhuru

Mjadala katika sehemu hii uliongozwa na mhimili wa vita vya baada ya uhuru. Kwa mujibu wa mwandishi Momanyi, kupigana na ufisadi kunahitaji kutokuwa na ubinafsi wala tamaa yoyote ile. Hili analidhihirisha kupitia ushirikiano na ukakamavu katika vita vya kujikomboa kutoka kwenye utando wa ufisadi. La msingi ni kujiua kitamaa na kuweka umoja na maendeleo ya taifa mbele. Akina Lonare, Sagura Sauni, Mrima, Mwamba na Mbaji wanamrejeshea Sagilu mlungula wa shilingi elfu mia nane na kukemea ubinafsi na utovu wa maadili ya akina Lonare yasiyotetereka. Ngoswe anajiunga nao na kuhama chama cha akina Sagilu na babake – Mtemi Lesulia.

Mhusika Cheiya licha ya kuwa na tamaa ya pesa anajizoazoa kiuchumi kwa kuimarisha usuhuba kati yake na Sagilu. Uhusiano kati ya Cheiya, Mashauri na

Sagilu kwa wakati mmoja unaashiria uhusiano kati ya bara la Afrika na mataifa kwasi ya Ulaya, Marekani na Asia. Hakika, kutokana na rasilimali asilia chungu nzima zinazopatikana barani Afrika pamoja na uwezekano wa bara la Afrika kuwa tajiri kuliko taifa wala bara lingine ulimwenguni, Afrika hutongozwa na mataifa ya ulimwengu wa kwanza. Yote hung'ang'ania kupata uhondo wa Afrika (Thiong'o, 2009).

Katika mataifa mengi barani Afrika, maandamano yamekuwa tukio la kawaida kutokana na kutamalaki kwa ukoloni mamboleo unaorejelewa kama ujadi wa kisasa na mtunzi Momanyi. Mtunzi anadhihirisha hili katika riwaya ya *Nguu za Jadi* anapowachora wananchi wa Matango wakiandamana. Sababu kuu ya maandamano ilikuwa kulalamikia uchomaji wa makazi yao kwa lengo la kuwafukuza wahamie kwingine. Hakika, dhiki na matatizo yanayowakumba wananchi huwaondolea imani yao juu ya uongozi na utawala. Hii ndiyo sababu wananchi wa Matango wanasusia kulindwa na polisi. Mkuu wa polisi anaelezwa na akina Sauni: "Hatuna haja ya ulinzi wako. Tutalindwa na Mwenyezi Mungu. Tokomea!" (uk. 76).

Vikaragosi hushabikia ubadhirifu wa mali ya umma na huwa mstari wa mbele kuwaibia wananchi mashamba yao. Ingawa mataifa mengi yaliyowahi kutawaliwa na kumilikiwa na mkoloni huwa huru, uhuru wenyewe huwa utumwa ndani ya ukoloni mamboleo (Bay, 2020). Mathalani, wananchi wa Matango wanachomewa makazi na baada ya siku chache wanatishwa kuondoka katika eneo lile kwa kisingizio cha ujenzi wa soko kuu la wachuuzi. Mtemi Lesulia yuko mstari wa mbele kuwadhulumu wananchi wake. Anamsisitiza Sagilu akisema: "Kwa vyovyote vile, hakikisha kwamba jalada la ardhi hiyo halipatikani. Sawa?" (uk. 78). Alitumia vitisho na maangamizi kama njia ya kuwanyamazisha na kuwadhibiti wananchi wake. Kutokana na haya, wananchi wanachukua sheria mikononi mwao na kuamua kuteketeza gari lililowaleta vijana wakiwa na mitungi na vibuyu vya mafuta ya petroli pale eneo la Matango usiku nyumba zilipochomwa.

Sagilu anapotoka ikulu akielekea Matango, anakuta umati wa watu umelizingira lile gari jekundu la Sihaba likiwa limeteketea nusu. Anabwabwaja maneno lakini hakuna anayemjibu. Wote wanamwangalia macho tu. Ghadhabu ya raia inafurika na kutiririka hadi kwenye kituo cha polisi ambapo wanadai kuachiliwa kwa Sihaba ili wamwadhibu ipasavyo. Sihaba anaonekana ameshikilia vile vijikaratasi vya kusambaza chuki mikononi. Lile shambulio dogo walilompa la kichapo cha mbwa halikuwaridhisha raia. Sihaba anatiwa ndani nao raia wanalazimishwa kuondoka pale kituoni na askari polisi. Katika vita vya kujikomboa kutoka kwenye utumwa wa ukoloni mamboleo, watu wengi wanaamini kuwa wenyewe ndio walio na uwezo wa kujikomboa kwani hawana imani na serikali. Mtunzi Momanyi anaonesha hili kupitia mhusika Mangwasha anapoeleza: "Dhuluma hii lazima

ikomeshwe. Na sisi wenyewe ndio tutakaoikomesha. Tusitegemee serikali" (uk. 80).

Mahakama ni ala nyingine wanayotumia baadhi ya wananchi kupigania uhuru wao. Hili linaoneshwa kupitia uamuzi wa wenyeji wa Matango wa kupeleka kesi ya kutetea ardhi yao mahakamani. Kwa mujibu wa Mtemi Lesulia, ardhi ile ya Matango ni mali ya Nanzia na Mbwashu. Huu ni ulaghai na unyang'anyi wa ardhi ya umma ambao huwa tukio la kawaida barani Afrika. Katika kesi hiyo, upande wa serikali unawakilishwa na mwanasheria fisadi mkuu, Bwana Mafamba, aliyehusika na kutoweshwa kwa majalada na nyaraka muhimu zilizohusu kesi za ufisadi nchini Matuo. Wananchi wa Matuo wanawakilishwa na Mwamba. Baada ya pande zote mbili kusikilizwa na hakimu, uamuzi unaowapa wananchi wa Matuo ushindi unatolewa: wote waliochomewa makazi yao wanatakiwa kujengewa nyumba zao upya kwa gharama ya serikali.

Vijana barani Afrika wanajitahidi kupigana na uongozi na utawala dhalimu kwa kubadilisha uongozi unaopalilia na kuimarisha ukoloni mamboleo. Kwa mujibu wa Mashauri akimjuza Lombo, uongozi uliopo huwajali wananchi hasa watoto, vijana na kina mama katika jamii ya Matuo. Aidha, Mashauri na Lombo wanapania kuwaondoa viongozi waliovimba vichwa kama Mtemi Lesulia, Sagilu na viongozi wenzao. Lombo anasisitiza kuwa kuna haja ya kuwaondoa viongozi wanaowadidimiza wananchi katika mashimo ya maradhi, uhitaji na ulitima wa kiajabu. Lengo kuu la kuwabadilisha viongozi kupitia upigaji kura ni kupunguza walalahoi kwa kuwapa mbinu za kujiendeleza kiuchumi. Vijana wa nchi ya Matuo wenye nia ya kujikomboa kutoka kwenye silisili za ukoloni mamboleo wanapigia upatu Chama cha Ushirika huku wakiwahamasisha vijana kuhusu haja ya kuukemea uongozi dhalimu. Viongozi wa taifa la Matuo hawawajali wananchi kamwe. Ngoswe anaeleza kuwa, Sagilu kama kiongozi ni mwewe ambaye hunyemelea vifaranga.

Wananchi wanajizatiti kuubomoa ukabila, ubinafsi na chuki kwa kuwang'atua viongozi dhalimu kutoka mamlakani. Vita vyao vya uhuru vinatekelezwa kupitia upigaji kura wa haki, uwazi na usawa. Ingawa viongozi dhalimu hawaamini kuwa uchaguzi unaweza kuwabandua uongozini kama anavyothibitisha Chifu Mshabaha, Mangwasha anasisitiza kuwa wananchi ndio serikali na wana uwezo wa kumchagua au kumtoa kiongozi yeyote yule kupitia upigaji kura wa wazi, usawa na haki. Viongozi dhalimu huimarisha ulofa katika taifa. Hii ndiyo sababu Chifu Mshabaha anawarejelea wananchi kama mafukara wasio mbele wala nyuma. Kwa hakika, viongozi dhalimu kando na kupalilia ufukara huendeleza ubaguzi na ukabila.

Ulofa huu huendelezwa kupitia sera dhaifu za uongozi na utawala zisizowajali wananchi. Wanaopata madhara zaidi ni watoto na vijana. Mathalani, nchi ya

Matuo imesheheni vijana wa mitaani ambao kulingana na Mangwasha ni kizazi kinachopotea. Kizazi hiki kipya kinaangamizwa taratibu na vikaragosi wa ukoloni mamboleo. Baadhi ya vijana wametimiza umri wa kuoa lakini hawawezi kujisimamia wenyewe. Wengine wamehitimu vizuri sana katika masomo lakini kutokana na ukosefu wa ajira na ulitima uliokithiri miongoni mwa wazazi wao, wanaishia vichochoroni wakiombaomba. Wengine wanavuta bangi na kupora mali za watu. Hili linasisitiza haja ya wananchi kupigania uongozi mwema unaowajali.

### 3.6 Ufisadi

Mjadala katika sehemu hii uliongozwa na mihimili ya ukoloni mamboleo pamoja na vita vya baada ya uhuru. Ufisadi unapalilia na kuendeleza uongozi dhalimu (Andersson na Anechiarico, 2019; Roberg na Hampson, 2024). Hili linahatarisha maisha ya watu wote wakiwamo watoto wadogo. Mathalani, Sagilu anaagiza maziwa ya watoto kutoka nje ya nchi yanayohatarisha maisha ya watoto wote nchini. Hii ni kwa sababu maziwa yenyewe yalikuwa na dawa yenye sumu iliyozuia maziwa kuharibika. Haya yote yanafanikishwa na ufanisi wa ufisadi nchini Matuo. Sagilu hakuwa na wa kumzuia kutekeleza ukatili huu. Hii inamaanisha kuwa alikuwa ameimarisha mtandao wa mafisadi ambao uliwapiku polisi. Ili kuimarisha uongozi dhalimu kupitia ufisadi, inawabidi viongozi wengi barani Afrika kutoa tishio la kuwaachisha kazi wanaojaribu kujikomboa kutoka kwenye matatizo ya ufisadi. Tamaa ya ukupe na ukunguni inapalilia uongozi mbaya.

Sagilu pamoja na viongozi wengine wananajisi uongozi kutokana na tamaa yao. Hili linawafanya waweze kumiliki mali na pesa zaidi kuliko serikali yenyewe. Sagilu, kwa mfano, anamiliki mashamba mengi, vituo vingi vya petroli na maduka chungu nzima ya jumla. Hivyo, matokeo yake ni ulofa uliokithiri. Baadhi ya madhara ya ulofa huu ni vijana kujitumbukiza kwenye dimbwi la ulevi, uraibu wa dawa za kulevya na anasa. Mathalani, Mrima anatumia vijisenti anavyopata kama mshahara kununua pombe haramu. Anaitelekeza jamaa yake na kujisahau. Kutokana na ulevi, vijana na wazee wanakumbatia uchafu na wadudu kama chawa katika maisha yao ya kila siku. Watoto ambao hawahudhurii masomo shuleni wanakosa maadili. Wanavaa mararu huku baadhi yao wakivuta vipande vya sigara vilivyotupwa na wapita njia. Mangwasha anajiuliza: “Je, hawa wangeweza kuwa raia wa kuaminika kesho kweli?” (uk. 34). Vibanda vya wagema vimo kwenye eneo lenye tope, maji taka, matapishi, mkojo na vinyesi aina aina vya binadamu.

### 3.7 Athari za Kumsahau Mtoto wa Kiume katika Uongozi na Maendeleo ya Jamii

Mjadala wa sehemu hii uliongozwa na mhimili wa uhuluti. Kwa mujibu wa mtunzi Momanyi, mtoto wa kiume amesahauliwa na jamii hasa barani Afrika. Hali hii imezalishwa na uigaji bubu pamoja na uhuluti wa utamaduni wa kigeni kwa ule wa Mwafrika. Hakika, katika juhudi za kusukuma usawa wa kijinsia, jamii nyingi

hasa za Afrika zimetia mkazo mkubwa kwenye kumtunza mtoto wa kike huku zikimpuuza mtoto wa kiume na mahitaji yake. Kwa ujumla, utamaduni wa Mwafrika unasisitiza kuwa wavulana wana uwezo wa kujisimamia kuliko wasichana kiuchumi, kisiasa na kijamii. Imani hizi zimesababisha kipindi ambacho kinatawaliwa na ukosefu wa mipango na sera za kumwezesha mtoto wa kiume. Hivyo, mtoto wa kiume ameachwa bila msaada wa kijamii, kijinsia na hata sheria zinazobuniwa zinamwonea mtoto wa kiume.

Matokeo ya kumtelekeza mtoto wa kiume ni viongozi wadhalimu, jamii isiyojielewa na malezi yasiyo na uwiano (Chang'ach, 2012). Hivyo, athari za kumsahau mtoto wa kiume husababisha madhara makubwa kwa maendeleo yake binafsi, ya jamii na uongozi kwa ujumla. Kupitia mhusika Mangwasha, mwandishi Momanyi anafafanua:

> Ole wako ewe mwanamume uishiye leo. Unayechakura mapipa ili kuizima njaa. Uliikosea nini jamii hata usalie kuwa ombaomba? … I wapi jamii isiyothamini elimu na utu wako? Jamii ilimshika mkono mtoto wa kike. Ikapiga mbio na mtoto wa kike (uk. 138).

Mzunguko wa dhiki, maradhi yanayoweza kuepukika pamoja na ukosefu wa usalama ni baadhi ya athari za kumsahau mtoto wa kiume katika uongozi na maendeleo ya kijamii. Hili linawiana na kauli ya Mortola na wenzake (2008), Reidd-Pharr (2022) na Pinkett (2023) kuwa, uongozi mbaya hupaliliwa na utelekezaji wa mtoto wa kiume katika jamii kwa lengo la kuimarisha ubeberu wa kisasa. Wataalamu tajwa wanapendekeza haja ya kutambua athari hizi na kuchukua hatua za kumuauni mtoto wa kiume kwa kumpa malezi sahihi yenye usawa, haki na ukweli ili kuimarisha mustakabali wake na maendeleo ya jamii. Mrima anathibitisha kuwa mtoto wa kiume amesahauliwa na jamii lakini amemezwa na anasa na ulevi kwenye ulimwengu wa malofa. Kutokana na utelekezi wa mtoto wa kiume, viongozi wabaya serikalini wanaibuka na hili linasababisha sera mbaya kwa ujumla. Hakika, haya yanachangia kumlemaza mtoto wa kiume zaidi.

Upuuzaji wa mtoto wa kiume unasababisha wavulana wengi kurandaranda mitaani kutokana na ukosefu wa malezi bora, umaskini wa wazazi wao na ukosefu wa karo. Kwa mujibu wa mtunzi Momanyi hakuna wazazi wa kiume wa kuwaongoza na kuwashika mkono wavulana hao ili wawe wanaume wa kutegemewa kwenye jamii na katika uongozi. Idadi kubwa ya wanaume inaishia kwenye ulevi kutokana na ukosefu wa matumaini. Suala hili linamaanisha kwamba umma wa kiume katika mataifa duni ulimwenguni kama vile ya Matuo umo hatarini na kizazi cha kiume cha kesho hakina matumaini.

**4.0 Hitimisho**

Makala haya yamejadili namna urithi wa vivuli unavyoanikwa kupitia nyuzi za baada ya ukoloni katika riwaya teule. Uhakiki wa makala haya uliongozwa na nguzo tatu za Nadharia ya Baadaukoloni. Clara Momanyi amefanikiwa kuwasilisha maudhui yake kwa hadhira lengwa kwa njia mwafaka na stahiki kupitia mjadala kuhusu ukoloni mamboleo, uongozi mbaya, ufisadi, unyamazishaji na vita vya baada ya uhuru. Haya ameyasawiri peupe kupitia wahusika wanaosawiri ukoloni mamboleo kama vile Mtemi Lesulia, Sagilu na Chifu Mshabaha. Vitendo, sifa na namna wahusika hao wanavyoumbwa na mwandishi vinaashiria usanii unaonuia kuanika vivuli vya baada ya ukoloni. Unyamazishaji unadhihirika kupitia mhusika Mtemi Lesulia, Sagilu, Chifu Mshabaha na vimada kama vile Sihaba na Cheiya. Unyamazishaji huu unajikita katika nyanja zote za maisha ya binadamu kama vile za kisiasa, kitamaduni, kiuchumi na kijamii. Unyamazishaji umeweza kujadiliwa kwa kuongozwa na mhimili wa ukoloni mamboleo. Hii ndiyo sababu jamii pana ya ulimwengu inamsahau mtoto wa kiume kama zao la unyamazishaji. Makala haya yananuia kuwa na mchango kwa kanoni ya kibaada ukoloni na masomo ya kibaada ukoloni kwa ujumla.

**Marejeleo**

Amis, P. (2020) “Key Themes in Contemporary African Urbanisation”. Katika P. Amis na P. Loyd (Wah.) *Housing Africa’s Urban Poor* (Toleo la 1). London: Routledge. kur. 1 – 34.

Andersson S. na Anechiarico, F. (2019) *Corruption and Corruption Control Democracy in the Balance* (Toleo la 1). London: Routledge.

Macleod, J. (2020) “Racism, Resistance, and the Origins of the Holmes County Movement”. Katika T. Bay (Mh.) *Minds Stayed On Freedom The Civil Rights Struggle In The Rural South-an Oral History* (Toleo la 1). New York: Routledge.kur. 1-17

Bennett, A. na Royle, N. (2024) *This Thing Called Literature Reading, Thinking, Writing* (Toleo la 2). New York: Routledge.

Blouin, K. na Akrigg, B. (2024) “Anti/post/de colonialism/coloniality: In Theory and In Practice”. Katika K. Blouin na B. Akrigg (Wah.) *The Routledge Handbook of Classics, Colonialism, and Postcolonial Theory* (Toleo la 1). London: Routledge. kur. 1 – 42.

Brear, M. (2020) “Silence and Voice in Participatory Processes – Causes, Meanings and Implications for Empowerment”. *Community Development Journal*, Juz. 55(2). Inapatikana katika https://doi.org/10.1093/cdj/bsy041. Ilisomwa tarehe 20 Aprili 2024.

Cardina, M. (2024) “Portugal, Colonial Aphasia and the Public Memory of War”. Katika M. Cardina (Mh.) *The Portuguese Colonial War and the African Liberation Struggles Memory, Politics and Uses of the Past* (Toleo la 1). Coimbra: Routledge. kur. 16 – 30.

Chang'ach, J.K. (2012) "Raising a Collective Voice to Address the Crisis of Boy-Child." *International Journal of Academic Research in Bussiness and Social Sciences*. Juz. 2(10): 34 – 45.

Coghe, S. (2017) "Reordering Colonial Society: Model Villages and Social Planning in RuralAngola, 1920 – 45." *Journal of Contemporary History*. Juz. 52 (1). Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/26416511. Ilisomwa tarehe 10 Julai 2024.

Dewald, C. (2002) "Narrative Surface and Authorial Voice in Herodotus' Histories". Katika G. Nagy (Mh.) *Greek Literature in the Classical Period: The Poetics of Drama in Athens* (Toleo la 1). London: Routledge. kur. 7 – 10.

Engbersen, G. (2020) *Cultures Of Unemployment A Comparative Look At Long-term Unemployment And Urban Poverty* (Toleo la 1). London: Routledge.

Falola, T. (2024a) *Daily Life in Colonial Africa (*Toleo la 1). London: Bloomsbury Publishing.

Falola, T. (2024b) *Chinua Achebe Narrating Africa in Fictions and History* (Toleo la 1). London: Bloomsbury Publishing.

Galperin, L.B. na Scheepers, B.C. (2025) *Essentials of Leadership in Africa* (Toleo la 1). London: Routledge.

Gandhi, L. (2020) *Postcolonial Theory A critical introduction* (Toleo la 1). Melbourne: Routledge.

Gibson, S. (2006) "Beyond a 'Culture of Silence': Inclusive Education and the Liberation of 'Voice'. *Disability and Society*, Juz. 21(4). Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/09687590600679956. Ilisomwa tarehe 16 Julai 2023.

Guohua, Z. (2023) *Literature and Power A Critical Investigation of Literary Legitimacy* (Toleo la 1.). London: Routledge.

Harris, R. K. (2024) *Misinformation, Content Moderation, and Epistemology Protecting Knowledge* (Toleo la 1). New York: Routledge.

Helgesson, S. na Thomsen, M. (2020) *Literature and the World* (Toleo la 1). London: Routledge.

Jacobs, R. (2020) *Literature in Our Lives Talking About Texts from Shakespear to Phillip Pullman* (Toleo la 1). London: Routledge.

Johnston, D., Deane, K. na Rizzo, M. (Wah.). (2019) *The Political Economy of HIV in Africa* (Toleo la 1). London: Routledge.

Jones, C. (2022) *Urban Economy Real Estate Economics and Public Policy* (Toleo la 1). London: Routledge.

Kamrava, M. (1999) *Politics and Society in the Developing World* (Toleo la 2). London: Routledge.

Kar, D. (2024) *Conflict Zone Literatures A Genre in the Making* (Toleo la 1). New York: Routledge.

Knight, G. K. (2020) *Unemployment An Economic Analysis* (Toleo la 1.). London: Routledge.

Koobak, R., Tlostanova, M. na Suruchi, T. (2022) "Uneasy Affinities Between the Postcolonial and the Postsocialist". Katika R. Koobak, M. Tlostanova na T. Suruchi (Wah.) *Postcolonial and Postsocialist Dialogues Intersections, Opacities, Challenges in Feminist Theorizing and Practice* (Toleo la 1). London: Routledge. kur. 4 – 12.

Loh, L. na Sen, M. (2018) "Postcolonial Literature and Challenges for the New Millenium". Katika L. Loh na M. Sen (Wah.) *Postcolonial Literature and Challenges for the New Millennium* (Toleo la 1.). Oxon: Routledge. kur. 1 – 4.

Loomba A. (2015) *Colonialism/Postcolonialism*. New York: Routledge.

Malcolm, S. (2024) *Age Discrimination Ageism in Employment and Service Provision* (Toleo la 1). London: Routledge.

Momanyi, C. (2021) *Nguu za Jadi*. Nairobi: Queenex Publishers Limited.

Mortola, P., Hiton, H. na Grant, S. (2008) *BAM! Boys Advocasy and Mentoring A Leader's Guide to Facilitating Strengths – Based Groups for Boys – Helping Boys Make Better Contact by Making Better Contact with them* (Toleo la 1). London: Routledge.

Muhammad, A. A., Muahammad, Z. R., Wajid, U. Muhammad, A. na Hamad, R. A. (2023) "Effect of Heavy Metal Polluted Soil on Physiology and Biochemistry of Plants". Katika T. Aftab na R. K. Hakeem (Wah.) *Environmental Pollution Impact on Plants Survival Strategies under Challenging Conditions* (Toleo la 1.). Oakville: Apple Academic Press. kur. 1 – 24.

Mwirabua, A.K. (2014) *Ukoloni Mamboleo na Utandawazi katika Tamthilia Teule*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Nanda, M. (2025) *Postcolonial Theory and the Making of Hindu Nationalism* (Toleo la 1). New Delhi: Routledge.

Oliver, L. (2016) *The Postcolonial Intellectual: Ngugi wa Thiong'o in Context*. New York: Routledge Taylor and Francis Group.

Omolo, K. (2002) "Political Ethnicity in the Democratisation Process in Kenya." *African Studies*, Juz. Na. 61(2): 209 – 221.

Pinkett, M. (2023) *Boys Do Cry Improving Boys' Mental Health and Wellbeing in Schools* (Toleo la 1). New York: Routledge.

Reid-Pharr (2022) "Dinge". Katika P. Smith (Mh.) *Boys Masculinities In Contemporary Culture* (Toleo la 1.). New York: Routledge. kur. 42 – 54.

Rotberg, R.I. na Hampson, F.O. (2024) "Measuring Grand Corruption and Inventing New Legal Barriers". Katika R. I. Rotberg na F. O. Hampson (Wah.) *Grand Corruption Curbing Kleptocracy Globally* (Toleo la 1). London: Routledge. kur. 1 – 9.

Rubin, B. (1988) *Modern Dictators: Third World Coup Makers, Strongmen and Populist Tyrants* (Toleo la 2). London: McGraw-Hill.

Singh, J.G. (2021) "Mapping, Defining and Imagining the Postcolonial". Katika J. G. Singh na D. D. Kim (Wah.) *The Postcolonial World* (Toleo la 1). Los Angeles: Routledge. kur. 1 – 26.

Sioh, M. (2024) *Colonial Trauma and Postcolonial Anxieties The Haunted Choices of Economic Development* (Toleo la 1). Chicago: Routledge.

Thiong'o, N. (1987) *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature.* Harare: Zimbabwe Publishing House (Pvt.) Ltd.

Thiong'o, N. (2009) *Re-membering Africa*. Nairobi: East African Publisher.

Waithiru, A.K. (2019) *Matumizi ya Taashira Kuangaza Jiografia na Utandawazi katika Tamthilia za Zilizala na Sudana*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia, Nyahururu.

Waithiru, A.K. (2022) "Tathmini ya Binadamu na Mazingira katika Riwaya ya *Nakuruto*". *Mwanga wa Lugha:* Juz. 7(2): 163 – 171.

Waithiru, A.K. (2024) "Uamilifu wa Jiografia na Utandawazi Kitaashira katika Tamthilia ya *Zilizala." East African Journal of Swahili Studies.* Juz. 7(2). Inapatikana katika https://doi.org/10.37284/jammk.7.2.2430. Ilisomwa tarehe 5 Desemba 2024.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Pubishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi*, *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Yamamura, M. na Yu-Chieh, L. (Wah.). (2023) *Visual Representations of the Cold War and Postcolonial Struggles Art in East and Southeast Asia* (Toleo la 1). Hong Kong: Routledge.